

**TAARIFA YA MAENDELEO YA JENGO LA OFISI ZA HALMASHAURI NA UKUMBI  
WA MIKUTANO KUFIKIA MWAKA 2017/2018**

Husika na mada tajwa hapo juu,

Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ilijiwekea kipaumbele cha kujenga Ofisi za Halmashauri na Ukumbi wa Mikutano mwaka 2008/09. Mradi huu wa Jengo la ghorofa 2, ulikadiriwa kuwa na thamani ya Tshs 6,200,000,000.00 baada ya kufanya mapitio gharama hizo zilionekena kushuka hadi Tshs 5,473,420,508.00 hadi kukamilika kwake. Kufikia mwaka wa fedha 2011/12 Halmashauri ilikuwa imetumia jumla ya Tshs. 1,119,356,283.48 kwa hatua za awali za kujenga Msingi wa jengo lote, kufuta jamvi, kujenga Column za Chini pamoja na Umbile la Ukumbi na kupauliwa (Skeleton Structures or Frames) na hatimaye Mkataba kati ya Shabat Company Ltd na Halmashauri ya Wilaya ulivyunjwa kutokana na sababu zilizojitokeza. *Jedwali hapa chini linaonesha mwaka na malipo yaliyofanyika.*

| S/N | MWAKA WA FEDHA     | KIASI KILICHOLIPWA      |
|-----|--------------------|-------------------------|
| 1   | 2009/2010          | 525,683,286.20          |
| 2   | 2010/2011          | 88,400,306.00           |
| 3   | 2011/2012          | 505,272,691.28          |
|     | <b>Jumla Ndogo</b> | <b>1,119,356,283.48</b> |

Katika kuendeleza ujenzi huu, Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2012/13 na 2013/14 ilipokea Tshs. 1,000,000,000.00 yaani Tshs.500,000,000.00 kwa kila mwaka na Tshs 600,000,000.00 kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Halmashauri ya Wilaya ya Masasi iliingia Mkataba wa Pili na Mzinga Holding Co. LTD ambayo ni taasisi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (Serikali) wakiwa washindi katika tenda ya kumalizia jengo kwa Tshs **4,354,064,225.00**. Mkataba kati ya Halmashauri ya Wilaya na **Mzinga Holding Co. Ltd ya S.L.P 791. MOROGORO** uliingiwa kwa Mkataba namba **LGA/083/2014/2015/W/07** na **Mekon Architect Consult Ltd ya S.L.P 31924. DSM** kama Mtaalamu Mshauri ambaye alikuwa ameanza utekelezaji wa kazi hiyo tangu Uchoraji, ujenzi hadi ilipofikia hatua ilipokuwa jengo limefikia.

**Hali ya Ujenzi kufikia sasa**

Ujenzi wa Ofisi za halmashauri na Ukumbi wa Mikutano upo katika hatua za umaliziaji kwa Ofisi za Chini pamoja na Ukumbi. Ambapo jumla ya Tshs **1,628,883,652.86** (Tshs **1,599,000,000.00** Serikali Kuu na Tshs **31,996,202.38** Mapato ya Ndani) zimetumika hadi June, 2018 kutekeleza shughuli zifuatazo:- kujenga kuta za chini na kufunika juu kwa zenge jamvi, ripu, kuweka milango, tiles, rangi, alluminium, kufunga mfumo wa Umeme, Viyoyozi, Feni na hatimaye kuweka mfumo wa maji taka ndani ya jengo. Hata hivyo, Mkandarasi bado anaendelea na kazi ya kupaka rangi na Kumalizia ofisi za chini na ukumbi hadi kukamilika. Kiujumla, hali ya utekelezaji ni asilimia 43 na ujenzi unaendelea. Mtiririko wa malipo ya Mkataba wa awamu ya pili kwa fedha zilizopokelewa ni kama ifuatavyo:-

| Gharama ya Mradi<br>(Awamu II) | Mwaka<br>wa<br>Malipo | Fedha Pokelewa<br>mpaka sasa. | Fedha Tumika            | Fedha Bakia<br>kumalizia Mkataba |
|--------------------------------|-----------------------|-------------------------------|-------------------------|----------------------------------|
|                                | 2014/2015             |                               | 456,260,014.00          |                                  |
|                                | 2015/2016             |                               | 234,887,251.82          |                                  |
|                                | 2016/2017             |                               | 279,740,184.66          |                                  |
|                                | 2017/2018             |                               | 657,996,202.38          |                                  |
| <b>4,354,064,225.00</b>        |                       | <b>1,600,000,000.00</b>       | <b>1,628,883,652.86</b> | <b>2,725,180,572.00</b>          |

**Jumla ya Matumizi ya Mradi kwa awamu I&II ni Shilingi 2,748,239,936.34**